**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Pemba*
*13 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA
# SALAMU ZA POLE

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa salamu za pole kwa Mkuu wa mkoa wa Kigoma, Mhe. Balozi Simon Nyakoro Sirro, kufuatia vifo vilivyosababishwa na ajali mbili tofauti zilizotokea asubuhi ya leo, tarehe 13 Machi, 2026, katika Ziwa Tanganyika, mkoani humo.

Katika ajali ya kwanza, watumishi saba wa afya wamepoteza maisha baada ya boti iliyowabeba kutokea Kigoma kuelekea kijiji cha Kagunga, mpakani mwa Tanzania na Burundi, kupinduka na kuzama ziwani baada ya kukumbwa na upepo mkali. Watumishi hao walikuwa wanakwenda kutoa huduma za afya katika vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Kati ya waliofariki, watumishi wanne ni wanaume na watatu ni wanawake. Aidha, watu 14 wamejeruhiwa na wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mkoa ya Maweni, Kigoma. Wakati huohuo, jitihada za kuwatafuta watu wawili ambao bado hawajapatikana zinaendelea kufanywa na vyombo vya uokoaji.

Katika tukio la pili, wavuvi watatu waliokuwa katika mtumbwi Ziwa Tanganyika walipigwa na radi wakiwa ziwani, na kusababisha kifo cha mvuvi mmoja huku wawili wakijeruhiwa.

Rais Dkt. Samia amepokea kwa masikitiko taarifa za ajali hizo na kuziombea roho za marehemu pumziko la amani. Aidha, ametoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa wote waliopoteza maisha.

***"Ninatoa pole za dhati kwa familia, ndugu na jamaa wa wote waliopoteza maisha katika ajali hizi,"*** amesema Rais Dkt. Samia, na kuwatakia uponyaji wa haraka majeruhi wote.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia amewataka wananchi, hususan wanaotumia vyombo vya usafiri na kufanya shughuli za uvuvi majini, kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya matumizi ya vyombo hivyo, sambamba na mabadiliko ya hali ya hewa, ikiwemo upepo mkali na radi.

Shaaban Kissu
K.n.y. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu